JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE

14 SEPTEMBA, 2017

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA NANE TAREHE 14 SEPTEMBA, 2017

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Mhe. Job Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Joshua Chamwela
2. Ndugu Neema Msangi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(1) Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto aliwasilisha Mezani:-

Maelezo ya Waziri kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016).*

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mhe. Peter Serukamba aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Kamati ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016).*

(3) Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto aliwasilisha:-

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016).*

III. MASWALI

OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 96: Mhe. Fakharia Shomar Khamis

Nyongeza: Mhe. Fakharia Shomar Khamis

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 97: Mhe. Joel Mwaka Mwakanyaga

Nyongeza: Mhe. Joel Mwaka Mwakanyaga

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 98: Mhe. Susan Limbweni Kiwanga

Nyongeza: Mhe. Susan Limbweni Kiwanga

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 99: Mhe. Abdallah Dadi Chikota

Nyongeza: Mhe. Abdallah Dadi Chikota
Mhe. Nape Moses Nnauye

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Swali Na. 100: Mhe. Almas Athuman Maige

Nyongeza: Mhe. Almas Athuman Maige
Mhe. Sabreena Hamza Sungura

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Swali Na. 101: Mhe. Mary Pius Chatanda

Nyongeza: Mhe. Mary Pius Chatanda
Mhe. Kemilembe Julius Lwota
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Swali Na. 102: Mhe. Anne Kilango Malecela

Nyongeza: Mhe. Anne Kilango Malecela
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Swali Na. 103: Mhe. Twahir Awesu Mohamed (kny. Mhe. Yussuf Salim Hussein)

Nyongeza: Mhe. Twahir Awesu Mohamed

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 104: Mhe. Halima Abdallah Bulembo (kny: Kabwe Zuberi Zitto)

Nyongeza: Mhe. Halima Abdallah Bulembo

IV. MATANGAZO

A. WAGENI

(i) Wageni 2 wa Mhe. Anna R. Lupembe ambao ni Madiwani wa Manispaa ya Mpanda kutoka Katavi, Mpanda.

(ii) Wageni 4 wa Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis ambao ni Wanafunzi wa Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT) cha Dar es Salaam.

(iii) Wageni 3 wa Mheshimiwa Grace S. Kiwelu ambao ni Viongozi wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini kutoka Kilimanjaro wakiongozwa na Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini Ndg. Aman Golugwa.

(iv) Mgeni wa Mhe. Leonidas Gama – Diwani wa Viti Maalum kutoka Ruvuma, Mhe. Judith Erasto Mborogo.

B. MATANGAZO MENGINE

(i) Mhe. Margareth Sitta – Mwenyekiti wa TWPG aliwatangaza Wabunge wote wanawake kuwa kesho tarehe 15/9/2017 kutakuwa na Semina kuanzia saa 7.00 mchana mpaka saa 10.00 jioni.

(ii) Katibu wa Bunge aliwatangazia Wabunge wote kuhusu Uzinduzi wa Mradi wa kuwajengea Uwezo Wabunge (Mradi wa LSP II) leo saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Bunge. Hivyo Wabunge wabaki Ukumbini kwa ajili ya Uzinduzi huo.

V. MAELEZO YA SPIKA – KUHUSU TUHUMA ZA MHE. LEMA

Mhe. Spika alieleza Bunge juu ya Tuhuma zilizoelekezwa kwake na Mhe. Godbless Lema kupitia Mitandao ya Kijamii kuhusiana na Mhe. Kubenea kupelekwa katika Kamti ya Ulinzi na Usalama; kupelekwa Polisi kwa Mhe. Kubenea katika mzozo wake na Mhe. Shonza; na Kuhusu Matibabu ya Mhe. Lissu ni kwa nini atibiwe Nairobi na siyo India kama Spika ambayo huwa akitibiwa huko.

- Mhe. Spika alieleza kwa kirefu kuwa Mhe. Kubenea alipelekwa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ili kuishaida Kamati kwa yale anayoyafahamu kuliko kuongelea nje ya Bunge, wala hakuna tuhuma yoyotekwake. Pia alisema kuhusu ugonvi wa Mhe. Kubenea na Shonza wala Spika hamjui huyyo Mhe. Shonza kama inavyosemekana.

- Mhe. Spika alieleza Mlolongo mrefu na makubaliano yaliyofanyika mpaka kufikia Maamuzi ya Mhe. Lissu kutibiwa Nairobi kuwa, ni maombi ya familia yake ili wawe na amani na Mhe. Mbowe ndiye aliyeomba kwa niaba ya familia ya Mhe. Lissu na kwamba yote hayo yakifanyika Mhe. Lema hakuwepo.

- Aidha, mhe. Spika aliwataja baadhi ya Wabunge ambao walitibiwa India kama yeye, hivyo kutibiwa India ni stahili ya Wabunge wote na sio Spika tu, ila kwa habari ya Mhe.Lissu ni matakwa ya familia ya Mhe. Lissu. Aidha aliongeza kuwa Spika aliamua Bunge limchangie matibabu kwa kukatwa nusu ya posho ya Wabunge ya siku moja ambapo ilipatikana milioni 43 kumsaidia Mhe. Lissu katika matibabu.

- Mwisho Mhe. Spika alisema amemsamehe Mhe. Godbless Leman a kutoa wito kwa Wabunge wote wenye maoni yao kuyapeleka kwenye Kamati husika kuliko kuongelea huko nje. Akamalizia na neon " Arusha Deserves Better".

- Mhe. Naibu Spika (Tulia Ackson) aliongoza Bunge baada ya Spika kuondoka baada ya Maelezo yake.

VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016)* – ulisomwa Mara ya Pili.

- Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii – Mhe. Peter Serukamba aliwasilisha Maoni ya Kamati juu ya Muswada huo.

- Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto aliwasilisha Maoni ya Upinzani kuhusu Muswada wa Madaktari.

- Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia Muswada wa Madaktari kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Nyongo - CCM

VII. TANGAZO

(i) Wageni wa Mhe. Susan Kolimba – Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki – ambao ni watoto wake wawili.

2. Mhe. Mussa Bakar Mbarouk - CUF
3. Mhe. Dkt. Godwin O. Mollel - CHADEMA
4. Mhe. Dkt. Hamis Kigwangalla - Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
5. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto – Mhe. Ummy Mwalimu alihitimisha hoja yake.

VIII. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia Muswada wa Madaktari kifungu kwa kifungu na kuyapitisha paoja na marekebisho ya Serikali.

IX. BUNGE KURUDIA

Bunge lilirudia na Mhe. Naibu Spika alimwita Waziri wa Afya atoe Taarifa na hoja ili Bunge liamua kupitisha Muswada huo.

Naibu Spika alilihoji Bunge na Hoja ya Waziri wa Afya iliamuliwa na kuafikiwa.

Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 *(The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016)* ulipitishwa na Bunge na Kusomwa kwa Mara ya Tatu.

X. KAMATI YA SHERIA NDOGO (HOJA ZA KAMATI)

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo – Mhe. Daniel Mtuka aliwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa.

- Wachangiaji wa Kamati ya Sheria Ndogo:-

  1. Mhe. Aida Khenani - CHADEMA
  2. Mhe. Jenista Mhagama (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Walemavu)
  3. Mhe. Andrew John Chenge – Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Hoja ya Kamati ya Sheria Ndogo ilipitishwa na Bunge.

XI. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 7.35 Mchana Bunge liliahirisha mpaka siku ya Ijumaa, tarehe 15/9/2017 saa 3.00 Asubuhi.